pdfeducation.com

SEHEMU A: INSHA (alama 20)

1. *Andika insha isiyopungua kurasa mbili wala kuzidi kurasa mbili na nusu juu ya mojawapo wa vichwa vifuatavyo*:

(a) (wewe ni daktari) Umealikwa kuhutubia wanafunzi kuhusu ugonjwa wa ukimwi. Andika hotuba yako.

(b) Watoto wanaorandaranda mitaani wamesukumwa huko na jamaa zao. Jadili.

(c) Wewe ni katibu wa halmashauri inayosimamia shughuli za kilimo mkoani. Umepewa jukumu la kuchunguza matatizo yanayoathiri kilimo na kupendekeza njia za kukabiliana nayo. Andika ripoti yako.

(d) Eleza shida zinazoikumba nchi ya Kenya kiuchumi na upendekeze suluhisho zinazoweza kutolewa.

(e) Andika insha itakayomalizia kwa maneno yafuatayo.

" ... dunia kweli wakati wa sasa imefikia kilele cha maendeleo ya teknolojia".

SEHEMU B: UFAHAMU (alama 30)

2. *Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo.*

Wakale hawakukosea walipoamba kuwa ngoja ngoja huumiza matumbo. Kila mmoja wetu alishikwa na wasiwasi baada ya kutayarisha shamba na kila uchao mawingu yalionekana yakikusanyika na kukusanyana bila matokeo ya mvua.

Mzee Sifemoyo alikuwa **kisaka** kimaumbile. Hakuwa na kazi wala bazi lakini alijivunia kijishamba chake ambacho alishiriki kukilima. Ungekutana naye **mafungulia ng'ombe** amebeba jembe lake huku akipiga mluzi na kutabasamu kwa furaha. Suruali lake ambalo lilikuwa limezoea mwili lilijaa viraka makalioni na angejifunga mshipi kisaki kiunoni.

Mkewe mzee Sifemoyo alijizatiti vilivyo kufanya vibarua, si kuosha nguo, **kupiga deki** na hata kufyeka ili akidhi mahitaji ya watato wao. Wanakijiji wavivu waliwaonea wivu na wakati mwingine ungewasikia wakinong'onezeana, "Mmph! Huyu kibarua maskini anajifanya mkulima na ilhali watoto wake wanalala njaa. Pyu! na bibiye! kijakazi cha kuingiaingia majumba ya watu kuwarubuni!

Kwa kuwa Mungu hamwachi mja wake, siku ziligeuka kuwa miezi. Miezi ikabadilika kuwa miaka bila ya mvua. Mzee Sifemoyo na mkewe hawakuchoka kuomba dua na kufanya kazi kwa bidii. Ungemkuta Mzee Sifemoyo alasiri akipumzika chini ya mti huku jembe lake likimwangalia. Kwake uturi wa kila siku ulikuwa kijasho chembamba kilichomtiririka mithili ya maji mferejini.

Siku moja hali hii mbaya iliamua kujibu matarajio ya Mzee Sifemoyo. Ghafla bin vu mvua ilimwagika msobesobe. Wanakijiji wavivu walianza kutafuta majembe na mbegu angalau wakimbilie

pdfeducation.com

mashambani, lakini wapi! Mvua iliendelea kunyesha isiwape nafasi hata ya kutoka nje. Kweli iliwaletea **mshoro**!

Mzee Sifemoyo ambaye tayari alikuwa ameshapanda alipumzika kungojea mavuno ambayo aliyapata si haba. Mkewe Sifemoyo alishushia kwa kuridhika. Watoto wake walipata chakula chenye virutubishi kamili. Waliomwona kama mtu wa kurauni kwa majumba ya mikuruba walimwona na **kutahayari**. Aliacha kuwa mshitiri wa kila mja ambaye alitaka yaya wa kuvichezesha vijitoto vyao kwa miezi vikipumzika.

Bei ya vyakula iliruka kila uchao, kiasi kwamba wanakijiji wangeenda kumstajiri Mzee Sifemoyo awagawie angalau ukufi wa chakula. Wenye viriba vilianza kuwapungua huku wakijilaumu kuwa kumsimanga Mzee Sifemoyo kuliwafanya wakalie mguu wa kausha.

(a) Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. (alama 2)

(b) Ni kwa nini wanaozungumziwa katika taarifa walianza kupatwa na wasiwasi? (alama 1)

(c) Taja mambo mawili yanayoonyesha ufukara wa Mzee Sifemoyo. (alama 4)

(d) Toa sababu ya mkewe Sifemoyo kuamua kufanya kazi ya ujakazi. (alama 1)

(e) Ni shutuma zipi zilizotolewa na wanakijiji dhidi ya Mzee Sifemoyo na mkewe? (alama 2)

(f) Kulingana na taarifa, eleza mambo mawili yanayothibitisha ushirikiano wa Mzee Sifemoyo na mkewe. (alama 2)

(g) Manukato ya Mzee Sifemoyo yalikuwa yapi kulingana na taarifa? (alama 2)

(h) Mwandishi anamaanisha nini anaposema:

(I) "Mvua ilimwagika msobesobe"? (alama 2)

(II) Kumsimanga Mzee Sifemoyo kuliwafanya wakalie mguu wa kausha. (alama 2)

(i) Kunyesha kwa mvua mfululizo kulisababisha madhara gani? (alama 1)

(j) Thibitisha uvivu wa wanakijiji wanaozungumziwa katika taarifa. (alama 2)

(k) Taja mafanikio yaliyoletwa na kunyesha kwa mvua kwa familia ya Mzee Sifemoyo. (alama 3)

pdfeducation.com

(l) Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na muktadha: (alama 5)

(I) kisaka;
(II) kupiga deki;
(III) mshoro;
(IV) kutahayari;
(V) mafungulia ng'ombe.

(m) Andika methali inayoafikiana na kifungu cha mwisho cha taarifa. (alama 1)

SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA (alama 30)

3. (a) Sahihisha sentensi:

(I) Mahali aliofungua hakuona pesa zake. (alama 1)

(II) Hapa ndiko alipookota saa hii. (alama 1)

(b) Eleza maana ya:

(I) kulia ngoa; (alama 1)
(II) kuweka kimada. (alama 1)

(c) Ikiwa mtondo ni Jumamosi:

(I) leo ni siku gani?
(II) juzi ni siku gani?

(alama 2)

(d) Eleza tofauti ya sentensi hizi:

(I) Alimpatia soda na chupa. (alama 2)

(II) Alimpatia soda kwa chupa. (alama 2)

(e) Andika kwa udogo:

(I) Idara zimenunuliwa magari yasiyoweza kubeba watu watatu. (alama 2)

(II) Ndege wetu wana manyoya ya kupendeza. (alama 2)

(f) Tumia vihisishi vifuatavyo katika sentensi: (alama 2)

(i) simile;
(ii) hasha.

pdfeducation.com

(g) Eleza matumizi ya KA katika sentensi hii:

Nilienda dukani nikamwona, nikamsalimu na nikamtuma kwao. (alama 2)

(h) Andika kwa wingi:

(I) Mwizi alikata ua uliozungushwa kiwanjani na akabomoa ufa wa nyumba. (alama 1)

(II) Uyoga umechipuka shambani mwangu. (alama 1)

(i) Eleza maana ya:

(I) tahiri; (alama 1)
(II) tairi. (alama 1)

(j) Hawa ni kina nani?

(I) Anayesimamia watu shambani? (alama 1)

(II) Aliyeikimbia nchi yake kwa ajili ya matatizo fulani. (alama 1)

(k) Eleza maana mbili za sentensi:

Swaleh alimpigia Jane mpira. (alama 2)

(l) Sehemu hizi za mwili ni zipi?

(I) utosi; (alama 1)
(II) kiwiko. (alama 1)

(m) Onyesha kiunganishi katika sentensi hizi:

(I) Zaina alipofika aliniamkua. (alama 1)

(II) Licha ya kusoma kwa bidii alianguka mtihani. (alama 1)

SEHEMU D: MBINU NA VIFAA VYA KUFUNDISHIA

Jibu maswali yote. (alama 20)

4. (a) Katika utafiti wako umegundua kwamba watu katika wilaya yako hawajui umuhimu wa teknolojia haswa kwa upande wa mawasiliano. Huku ukitumia vifaa mwafaka, onyesha vile utatatua tatizo hili.

(b) Tarafa lako limekumbwa na visa vya uhalifu kutokana na msukosuko wa kisiasa. Umealikwa na chifu wa tarafa hili ili uwashauri wenyeji juu ya kudumisha amani. Kwa kutumia vifaa halisi, onyesha utakavyoshughulikia ujumbe huu.